HABARI LEO UK17.

# Bei ya nyama yapanda Dar

Na Lucy Lyatuu

BEI ya nyama katika bucha mkoani Dar es Salaam imepanda kwa kiwango kikubwa na kufikia kuuzwa Sh 10,000 kwa kilogramu.

Uchunguzi uliofanywa na HabariLEO, umeonesha kitoweo hicho kimepanda bei katika kipindi hiki cha kuelekea katika sikukuu za mwisho wa mwaka.

Akizungumzia hali ya bei ya nyama, daktari wa wanyama kutoka Bodi ya Nyama Tanzania, Olais Ngilisho alisema hawapangi bei elekezi ya bidhaa hiyo bali inaweza kupanda kwa sababu mbalimbali ikiwamo ubora wa nyama.

Alisema wadau wenyewe wa mifugo ndio wenye jukumu la kupandisha bei ya bidhaa hiyo lakini kwa kuzingatia ubora wa nyama husika na wakati mwingine hali ya upatikanaji.

Ngilisho alisema kuna kiwango cha wastani wa kuuzia nyama kuanzia Sh 6,000 hadi 10,000 kwa kilogramu moja ya nyama kutegemea ubora.

Aidha, alisema vipo vikao vya wadau husika ambao hukutana kupanga bei na katika biashara hiyo. Pia wapo wauzaji wa aina mbili ambao ni wafanyabiashara wadogo wanaouza nyama wakiwa na kilogramu kuanzia tano hadi 10 na wale wanaouza kwenye bucha kuanzia ng'ombe 20 na kuendelea.

Alisema miongoni mwao, wapo wadau wenye bucha ambao pia ni wachinjaji wanaoweza kupanga bei kulingana na thamani wanayoiona inafaa kwao.

Hata hivyo, alishauri wafanyabiashara kuacha tabia ya kupandisha kitoweo hicho hasa kwa sababu ya sikukuu za mwisho wa mwaka wakiamini kuwa ulaji huongezeka, bali wapange bei kutokana na ubora wa nyama husika na hali ya upatikanaji.

CamScanner

NIPASHE UK 21

## Kampuni yachochea ongezeko uzalishaji wa maziwa

**Na Grace Mwakalinga,**
RUNGWE

UPATIKANAJI wa mbegu bora za madume ya ng'ombe kwa wafugaji wilayani Rungwe, kumechochea ongezeko kwa uzalishaji maziwa kufikia zaidi ya lita 200,000 kwa siku na kuingizwa sokoni.

Mwenyekiti wa Muungano wa Chama cha Wafugaji wilayani Rungwe (MUHAMARU), Asha Lukaja, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na Nipashe kuhusu hatua walizochukua ikiwa ni siku kadhaa kupita baada ya kufanya kikao cha kujadili mambo ya kufanya ili kukuza uzalishaji wa maziwa wilayani humo.

Alisema mafanikio ya upatikanaji wa mbegu bora za madume ni kupata elimu ya kuzalishaji pamoja na masoko, kabla ya elimu hiyo walikuwa wakikabiliwa na tatizo la masoko na mbegu bora, kiwanda cha maziwa cha Asasi kimewapatia madume ya mbegu bora za ng'ombe ambayo yamesaidia ongezeko la majike ambayo yamekuwa kochocheo kikubwa cha ongezeko la uzalishaji maziwa.

"Licha ya ongezeko la uzalishaji wa maziwa na uwepo wa masoko ya uhakika bado tatizo kwa baadhi ya wafugaji kuingiza sokoni maziwa yasiyokuwa na ubora jambo linalochangia kuchafua na kutia doa maziwa yanayozalishwa wilayani Rungwe," alisema Lukaja.

Miongoni mwa wafugaji wilayani Rungwe, Fadhili Mbilinyi alisema kuwapo kwa kampuni ya ununuzi wa maziwa wilayani Rungwe kumeleta tija wa wafugaji kuongeza uzalishaji na kufuga kisasa.

Alisema kwa sasa wanazalisha kiasi kikubwa cha maziwa na uhakika wa upatikanaji wa soko ndani na nje ya wilaya hiyo.

Ofisa Mifugo Wilaya ya Rungwe, Dk. Dennis Kamily, alisema wafugaji wengi hawapendi kuwatumia maofisa ugani kujifunza namna bora ya kuzalisha maziwa bila kutumia vyakula visivyo salama kwa ng'ombe.

Mkaguzi wa Maziwa Wilaya ya Rungwe, Henry Mokiwa, alisema asilimia 20 ya maziwa yanayozalishwa na wafugaji wilayani humo yanakosa ubora kutokana na baadhi ya wafugaji kuongeza maji.

"Ukamuaji wa maziwa kiholela kwa baadhi ya wafugaji kunachangia kuzalisha bakteria 500 hadi 1,000 kila baada ya saa tatu na kusababisha madhara kwa watumiaji na kushauri wafugaji kuwatumia maofisa ugani ili kuboresha sekta ya maziwa nchini," alisema Mokiwa.

THE GUARDIAN Page 1.

# Board in markets drive as meat exports pick up



Zanzibar President Dr Hussein Ali Mwinyi receives a traditional basket from Dr Mwanahija Ali Juma, executive secretary for the Zanzibar Kiswahili Council, when visiting an entrepreneurs' exhibition to wind down the sixth International Kiswahili Conference in Wete, Pemba Island yesterday. Photo: State House

By Guardian Correspondent, Morogoro

TANZANIA has slightly increased meat processing and exports this year, with strategies being put in place to set foot in new markets.

Dr Daniel Mushi, the Tanzania Meat Board (TMB) registrar, said here at the weekend, that the country currently sells meat to the Middle East and a few countries in Africa and the Far East.

He said exports go to Qatar, UAE, Oman, Saudi Arabia, Bahrain, Jordan, Kuwait, Hong Kong, Vietnam, Kenya and the Comoros, with plans underway to further penetrate the Chinese market.

In five months from July to November, consignments adding up to of 4,374 tonnes of meat valued at $16.76m were shipped to these destinations, with 738,165.9 tonnes produced.

> **As of now we have captured foreign meat markets and we expect to start selling meat to China**

In fiscal 2020/21 production rose by 4.3 per cent to 769,966.6 tonnes, he said, elaborating that the sourcing of markets was contributed to by building newer abattoirs and meat processing plants.

In fiscal 2020/21, a total of 1,774 tonnes of meat was sold to various foreign markets, rising to 10,415 tonnes, more than quadrupling the tonnage, he said.

Considerable efforts by the government and private sector firms to look for new meat markets abroad brought about the massive uplift, he stated.

Setting up meat processing plants like the Nguru Hills Ranch spurred the growth of meat exports. The new ranch was formally inaugurated in Mvomero by the Livestock and Fisheries minister Mashimba Ndaki.

"As of now we have captured foreign meat markets and we expect to start selling meat to China following the recent visit of President Samia Suluhu Hassan to the country," he added.

# Experts: Schools need mental health advisers

By Correspondent James Kandoya

MENTAL health experts are recommending that counsellors be stationed in schools to guide pupils as it emerges that mental health problems among children and adolescents are on the rise.

Dr Samwel Likindikoki, a lecturer and medical psychiatry at the Muhimbili University of Health and Allied Sciences (MUHAS) issued this appeal at a panel discussion on child and adolescent mental health as part of the fourth national non-communicable diseases scientific conference.

He lamented that the schooling structure lacks counselling facilities despite that most adolescents face mental health problems, on the basis of

TURN TO PAGE 2

UHURU UK 2

# Ranchi yamegwa, wapewa wananchi

Na MWANDISHI WETU

SERIKALI imemega baadhi ya maeneo ya Ranchi ya Kagoma yenye ukubwa wa hekta 50,690 na kuyarasimisha kwa wananchi wa Kata ya Rutoro wilayani Muleba mkoani Kagera kwa shughuli za makazi, kilimo na ufugaji.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Kamati ya Mawaziri wa Kisekta katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika eneo la Shule ya Msingi Rutoro, Muleba.

Akizungumza katika mkutano huo, Mwenyekiti wa kamati hiyo ambaye ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (Mb), alisema maeneo hayo yatamegwa na kupewa wananchi kwa kuzingatia ushauri wa watalaamu.

"Maeneo yatakayomegwa kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu kutoka kwenye ranchi yatawekewa utaratibu wa usimamizi na uongozi wa mkoa ukishirikiana na wilaya ili msigombanie au kufanya jambo lolote ndani ya maeneo hayo," alisisitiza.

Ndaki aliwaonya viongozi wa vijiji na vitongoji kuacha tabia ya kugawa maeneo hayo kwa kuwa hawana mamlaka ya kugawa.

Katika hatua nyingine, Ndaki alisema serikali imeridhia kukiacha Kitongoji cha Rwamisha 'B' ambacho kilichopo Wilaya ya Karagwe chenye kaya 480 ambacho awali kiliamuliwa kiondoke.

Waziri huyo aliuelekeza Mkoa wa Kagera kuandaa mpango wa utekelezaji wa maamuzi ya Kamati ya Mawaziri ya Kisekta yaliyofikiwa ikiwa ni pamoja kurekebisha mipaka ya vijiji kwa kuzingatia maoni ya wataalamu.

SaNJARI na hilo, Waziri Ndaki aliwatoa

> **MAENEO**
>
> Yatakayomegwa kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu kutoka kwenye ranchi yatawekewa utaratibu wa usimamizi na uongozi wa mkoa ukishirikiana na wilaya ili msigombanie au kufanya jambo lolote ndani ya maeneo hayo.

hofu wawekezaji walioko katika ranchi ya Kagoma akiwaeleza kuwa wapo salama na serikali imefanya mazungumzo na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) uwekwe utaratibu mzuri ambao utawawezesha kupewa maeneo yatakayomegwa.

Aliwaasa wananchi kuwa watulivu wakati wa utekelezaji wa maamuzi ya kamati hiyo na kuacha kuvamia maeneo kurahisisha utekelezaji wa maamuzi hayo.

Naye, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, aliwataka wananchi kuendelea kuheshimu sheria za ardhi hususan katika mpango wa maendeleo ya ardhi na kwamba, kuna kazi ya kufanya katika kuhakikisha miundombinu na majengo ya eneo la Rutoro yanakaa sawa.

Alitoa rai wananchi hao kuwa watulivu mpaka wataalamu wa ardhi watakapokuja kutoa utaratibu wa maeneo yaliyoachiwa kwa wananchi.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, aliwataka wananchi wa Kata ya Rutoro kuitumia ardhi waliyoachiwa kwa maendeleo kwa kuanzisha miradi ya upandaji miti pamoja ufugaji nyuki.

"Nendeni mkapande miti kibiashara mtapata mbao na wakati huohuo mnaweza kuanzisha miradi ya ufugaji nyuki,'alisema Mary.

ANaibu waziri huyo alitoa wito kwa wananchi kutoyavamia maeneo yatakayoachwa kwa Serikali kwa kuwa ni maeneo yanayotunzwa kwa faida ya kizazi cha leo na kinachokuja.

Kamati ya Mawaziri wa Kisekta imehitimisha ziara yake mkoani Kagera na itaendelea na kazi hiyo mkoani Ruvuma.